


Chanjo ya mafua

Mafua husababishwa na virusi, ambayo huenea kwa urahisi sana na vinaweza kusababisha magonjwa makubwa kama vile nimonia. Ingawa watu wazee wana uwezekano mkubwa wa kuugua mafua, watoto pia wako hatarini, na chanjo ndiyo kinga bora zaidi.



Kuanzia msimu wa vuli, NHS inatoa chanjo ya mafua bila malipo kwa:


- Kila mtu mwenye umri wa miaka 65 na zaidi Watoto wenye umri wa miaka 2 na 3
- Watoto wenye umri wa kuanza shule hadi miaka 11
- Watoa huduma wa afya na huduma za kijamii
- Wajawazito
- wale ambao wapo karibu na watu wenye upungufu wa kinga
- Wale wenye umri wa miezi 6 hadi chini ya miaka 65 katika makundi ya kliniki yaliyo kwenye hatari (pamoja na wale walio na magonjwa sugu ya moyo, figo, ini na mfumo wa upumuaji)
- Wale walio katika nyumba za malezi kwa muda mrefu
- Wale ambao ni walezi wa karibu zaidi wa wazee au watu wenye ulemavu

Wasiliana na daktari wako wa kliniki, duka la dawa au uweke nafasi mtandaoni. Ikiwa hustahiki chanjo ya mafua bila malipo, unaweza kupata kwa kulipia katika duka dawa



Nilipata chanjo ya mafua mwaka jana; Je ninahitaji nyingine tena mwaka huu?

Ndio. Kwa ulinzi bora zaidi, unapewa chanjo ya homa kila mwaka katika vuli/msimu wa baridi wakati virusi vya mafua vinapoenea. Virusi vya mafua hubadilika mara nyingi sana na hivyo chanjo hiyo inaboreshwa kila mwaka ili kuendana na virusi vilivyopo.



Kwa nini watoto wengi wa shule wanastahili kupata chanjo ya mafua mwaka huu?

Mafua yanaweza kusababisha dalili mbaya na magonjwa kwa watoto na vijana, chanjo hutoa kinga bora dhidi ya virusi. Ni muhimu kuwaweka watoto wakiwa na afya nzuri ili kuhudhuria shule kama inavyowezekana. Kuchanja wanafunzi pia kunasaidia kupunguza kuenea kwa virusi kwa vikundi vilivyo hatarini zaidi, pamoja na wazee. Chanjo huwalinda watoto wa shule, familia zao, pamoja na marafiki.



**Chanjo ni kinga bora dhidi ya ugonjwa wa mafua.
Angalia ikiwa unastahiki kupata chanjo bure ili
kujilinda wewe na wengine!**